

MFUKO WA FIDIA KWA WAFANYAKAZI



TAARIFA KWA UMMA

Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi (WCF) unakanusha taarifa inayosambazwa katika mitandao ya kijamii yenye kichwa cha habari “TAARIFA MUHIMU”. Taarifa hiyo inadai kuwa ni maagizo kutoka Wizara husika kwamba kuna zoezi litakalofanyika hivi karibuni la watu wa idara ya kazi kupita nyumba kwa nyumba kufanya ukaguzi wa masuala ya kazi ikiwa ni pamoja na malipo ya WCF kwa wafanyakazi wote ikijumuisha wafanyakazi wa majumbani na kuainisha adhabu ya milioni 50 au kifungo cha miaka 5 kwa watakaokiuka.

Tunapenda kuufahamisha umma kuwa taarifa hizi si za kweli. Aidha, Mfuko unawataka watu wanaoeneza taarifa hizo za kizushi waache kufanya hivyo mara moja ili kuepusha usumbufu unaojitokeza. Hatua za kisheria zitachukuliwa kwa watakaobainika kuanzisha na kusambaza taarifa hizo.

22/09/2017

IMETOLEWA NA

KITENGO CHA MAWASILIANO

MFUKO WA FIDIA KWA WAFANYAKAZI (WCF)

S.L.P. 79655, DAR ES SALAAM

Barua Pepe: info@wcf.go.tz; Tovuti: www.wcf.go.tz